THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021** **KISWAHILI**
**(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

**MUDA: Saa 3** **2006/10/12 Asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B, C, D na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu E. Swali la **12** ni lazima.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
5. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

## UFAHAMU

1. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya swali.

Wa ubani Rawaziri, na Kandoro kadhalika,
Lumbano la kishairi, gazetini kuliweka,
Nami nimejikusuri, maoni kuyatamka,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Kutunzwa watu wa enzi, kwa ua sijaridhika,
Siyo zawadi azizi, hasa inoheshimika,
Bado hamjamaizi, kwa tunzo inosifika,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Ua kupewa harusi, **nikaha** inapofika,
Ni siku ya **taanusi**, kwa bibi kuheshimika,
Lakini ua ni tusi, kwa dume kulipachika,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Ua hupambwa maiti, jeneza likapambika,
Harufu kila wakati, haiba kuongezeka,
Na wengine hawataki, uchuro watatamka,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Ua huvishwa mgeni, mtukufu akifika,
Ni koja la asumini, shingoni linajiweka,
Mara utalibaini, walinzi wamelishika,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Ua tunzo ya mahaba, wapenzi wanohusika,
**Ishara ya usuhuba**, wawili kukutanika,
Lakini na makahaba, na wao hujipachika,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Ua kama lina hadhi, si wote wanaoridhika,
Wengine haliwakidhi, na hata kwa kulishika,
Sembe kwao ni **faradhi**, njaa itamwondoka,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.

Ua likiwa mtini, huwa linanawirika,
Huwa na kubwa thamani, hapo lilipojishika,
Likitiwa mikononi, si muda linanyauka,
Ua si **ruwaza** njema, tuzo ya mtu kupewa.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

**Maswali**

(i) Kichwa cha shairi hili chaweza kuwa

A Ruwaza
B Zawadi
C Ua si ruwaza njema
D Tuzo ya mtu kupewa
E Zawadi ya harusi.

(ii) Neno "nikaha" kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana ya

A pingu za maisha
B ndoa
C sherehe ya harusi
D siku ya taanusi
E siku ya majonzi.

(iii) Kulingana na habari hii watu wanaotakiwa kupewa zawadi ya ua ni

A watu wa enzi, wapenzi na maarusi
B maiti, bibi harusi, mgeni na wapenzi
C watu wa aina zote katika shughuli maalum
D bibi harusi pekee
E mgeni na maarusi.

(iv) Ubeti wa saba una maana kwamba

A watu wote hufurahishwa na zawadi ya maua
B zawadi ya maua si utamaduni wa mwafrika hivyo watu wengi hawaipendi
C badala ya zawadi ya maua kwa watu wengine ni bora ungewapa chakula
D sembe kwao ni faradhi, njaa itamwondoka
E ua si ruwaza njema.

(v) Neno "ruwaza" kama lilivyotumiwa na mwandishi lina maana ya

A zawadi B nia C adabu D tabia E nikaha.

(vi) Mwandishi anaposema "ishara ya usuhuba" ana maana ya

A ishara ya husuda
B alama ya ushirikiano wa wapenzi wawili
C ishara ya mapenzi
D dalili ya wivu
E tabia nzuri.

(vii) Mawazo makuu ya mwandishi katika shairi lake ni

A zawadi ya maua si nzuri sana kwani ni utamaduni wa kigeni na kiafrika pia
B zawadi ya maua hufaa kwa baadhi ya watu kwani wengine huona kama uchuro
C ua lina hadhi yake lakini sio wote wanaoipenda zawadi yake
D ua linafaa kwa maarusi tu
E zawadi ya ua haina hadhi yoyote.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

(viii) Neno "faradhi" kama lilivyotumiwa na mwandishi lina maana ya

A muhimu B fahari C ridhia D faida E lazima.

(ix) Mwandishi katika ubeti wa mwisho anasema kuwa

A si vizuri kuyakata maua kutoka mtini
B thamani ya ua ni pale linapokuwa mtini kwake
C anawalaumu watu wanaoyachuma maua
D maua huchumwa kisha kunyauka
E ua likiwa mtini ni ruwaza njema.

(x) Mwandishi anaposema "nimejikusuri" anamaanisha

A amejikusuru
B amejitupa uwanjani
C amejizuia
D amejihusisha
E amejinasua.

2. Unapofupisha habari unatakiwa kuzingatia mambo gani muhimu? Yataje mambo **matano (5)** na ueleze umuhimu wa kila jambo katika kufupisha habari.

## SEHEMU B (alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

## UTUMIZI WA LUGHA

3. Chagua kifungu cha maneno kutoka **Orodha B** kinachotoa maelezo sahihi ya maneno/neno katika **Orodha A**. Andika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya kipengele cha swali katika kijitabu chako cha kujibia.

| ORODHA A | | ORODHA B | |
|---|---|---|---|
| (i) | Hatua ya kwanza ya uchanganuzi wa sentensi | A | Sentensi nyofu |
| (ii) | Kanda | B | Ni kipashio cha kiarifu |
| (iii) | Shamirisho | C | Shule |
| (iv) | "Mofimu ni kiambishi" | D | Kuainisha maneno ya sentensi |
| (v) | Wingi wa shule | E | Mashule |
| | | F | Sentensi tata |
| | | G | Hukaliwa na maneno ya vitenzi |
| | | H | Usemi huu ni sahihi |
| | | I | Usemi huu si sahihi |
| | | J | Kuainisha sentensi |

4. Sentensi zifuatazo zina makosa. Ziandike vizuri kwa kuepuka hayo makosa yaliyojitokeza.

(a) Tulikaribishwa chai rangi na maandazi.

(b) Barua ulioniandikia ndiyo hii.

(c) Wasichana wa kike wanaitwa.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

(d) Tanzania nzima kwa ujumla itakabiliwa na njaa mwaka huu.

(e) Wote munaombwa mfike bila kukosa.

5. Eleza kwa kutoa mifano kuonesha rejesta inayotumika katika sehemu zifuatazo:

(a) Hotelini.

(b) Mahakamani.

(c) Sokoni.

(d) Hospitalini.

(e) Ndani ya mabasi.

## SEHEMU C (alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

### SARUFI

6. Istilahi moja inaweza ikawa na majina mawili. Andika majina mengine ya dhana zifuatazo:

(a) Chagizo.

(b) Shamirisho.

(c) Prediketa.

(d) Mofimu za wakati.

(e) Kuainisha.

7. Tumia neno "alikuwa" kuonesha:

(a) Kitenzi kisaidizi (TS).

(b) Kitenzi kishirikishi (t).

(c) Shina la neno "alikuwa".

8. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi kwa kutumia hatua **nne (4)** za uchanganuzi:

Mwalimu hodari atakuwa anafundisha vizuri.

9. Eleza kwa kutoa mifano dhima **tatu (3)** za viambishi.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (alama 10)

**Jibu swali la kumi (10)**

### HISTORIA YA LUGHA

10. (a) Taja maana **tano (5)** za mswahili.

    (b) Eleza shughuli za utawala wa wajerumani kabla ya uhuru zilizokuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania.

## SEHEMU E (alama 40)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii. Swali la **12** ni la lazima.

### FASIHI

11. Kwa kutumia mifano madhubuti, jadili vipengele vinavyoibainisha fasihi simulizi.

12. "Kufuatana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia nafasi ya fasihi andishi katika Tanzania ya sasa ni muhimu". Jadili kauli hiyo kwa kutumia vitabu **viwili (2)** vya ushairi vilivyoorodheshwa.

13. Kujikomboa ni kwa aina nyingi katika maisha ya binadamu. Eleza ukombozi huo ukithibitisha kwa mifano kutoka riwaya **mbili (2)** zilizoorodheshwa.

14. Eleza jinsi wahusika na mandhari wanavyoweza kujenga na kufikisna ujumbe wa kazi ya fasihi kwa wasomaji kwa kutumia tamthiliya **mbili (2)** zilizoorodheshwa.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| DIWANI YA MLOKA | - | C. MLOKA (B.P) |
| MASHAIRI YA CHEKACHEKA | - | T.A. MVUNGI (EDP) |
| MALENGA WAPYA | - | TAKILUKI (DUP) |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| KUSADIKIKA | - | S. ROBERT (E.P) |
| WATOTO WA MAMA NTILIE | - | E. MBOGO (H.P) |
| KIU YA HAKI | - | Z. MWANGA (R.P) |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| NGOSWE-PENZI KITOVU CHA UZEMBE | - | E. SEMZABA (ESC) |
| MFALME JUHA | - | F.M. TOPAN (DUP) |
| KILIO CHETU | - | MEDICAL AID FOUNDATION (TPH) |



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org